# KENYA NATIONAL EXAMINATION COUNCIL
# REVISION MOCK EXAMS 2016
## TOP NATIONAL SCHOOLS

**MOI GIRLS ELDORET**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 3**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**SCHOOLS NET KENYA**
Osiligi House, Opposite KCB, Ground Floor
Off Magadi Road, Ongata Rongai | Tel: 0711 88 22 27
E-mail:infosnkenya@gmail.com | Website: www.schoolsnetkenya.com

# MOI GIRLS ELDORET KCSE TRIAL AND PRACTICE EXAM 2016

**102/3**

**KARATASI YA 3**

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

1. (a) Je, mashairi haya mawili ni ya aina gani.

A – huru – halijazingatia arudhi za utunzi wa ushairi.

B – tarbia – lina mishororo 4 katika kila ubeti.

- Kikwamba – neno 'dunia' laanzia kila mishororo.
- Mtiririko – vina vya kati na mwisho vina keketo.
- Mathnawi – kila mshororo una vipande viwili.
- Shairi la arudhi kwa sababu limezingatia arudhi za utunzi wa ushairi. *Kutaja na kueleza.*(alama 2)

(b) Taja dhamira kuu katika kila shairi.

A - Kukashifu viongozi wanaouwatesa wafanyakazi.

- Kuangazia haki duni ya ufanyakazi mikononi mwa waajiri katili.

B - Kuangazia jinsi binadamu afaa kutahadhari na dunia inayo dhuru / angamiza. (Hoja 1x2 = 2)

(c) Kulinganua mashairi haya kiumbo.

| A | B |
|---|---|
| (a) lina beti 4 | - lina beti 4 |
| (b) idadi ya mishoro kila ubeti ni tofauti | - kila ubeti una mishororo 4 |
| - vina vyatofautiana kwa kila ubeti | - vina vina keketo |
| - halina kibwagizo | - lina kibwagizo maalum |
| - mishororo haija gawika vipande vipande | - limegawika kuwili ukwapi na utao |
| - mizani yatofautiana kwa kila mshororo | - mizani ni sawa 8,8 |

*Tatu za kwanza – kila hoja lama 1 x 3 = 3*

(d) **Nafsi nenewa katika mashairi haya mawili**.

A – Mwajiri katili anayewadhulumu wafanyakaziakijitajirisha kwa jasho lao.

B – binadamu asiyetahadhari na dunia. *Kila hoja alama 1 x 2*

(e) **Matumizi ya mbinu hizi za kimtindo katika shairi la A**.

(i) Kweli – kinzani - kilio kisichokuwa na machozi.
- barabara zisizokuwapo.

(ii) Mishata - utazame mlolongo wa
- watokwao na jasho kapakapa na
- wanaotafunwa uhai na jua liso. *Ya kwanza al. 1 x 2*

(f) Tabdila badala ya waichezee – kupata urari wa vina 'ye'
Kutaja na kueleza umuhimu – alama 1

(g)

| A | V |
|---|---|
| - Kazi inawala chenga | - dunia kama tapeli inahadaa |
| - Wanatafunwa uhai na jua | - dunia inampiku mwenye akili |
| | - dunia yapika majungu |

(alama 2)

(h) Ubeti wa tatu katika shairi la A kwa lugha nathari.
Pia mchunguze maskini na mapato ya kazi yake duni, yasiyotosheleza mahitaji yake, na anayevalia nguo zilizochanika na zisizosetiri mwili usio na nguvu, na hulia bila kutokwa na machozi. (hoja zozte 4x1 = alama 4)

(i) Maana ya msamiati.
(i) Inampiku – inamshinda / inamweza
(ii) Makontena – shehana / mizigo mizito / makasha. (hoja 2x1 = alama 2)

2. (a) (i) Msemaji ni Daktari Siki.
(ii) Anayesemewa ni Tatu mmoja wa wawakilishi wa wafanya kazi.
(iii) Wako katika ofisi ya Daktari Siki.

(iv) Tatu amekuja kumwona na kumsihi Daktari Siki aende aseme na Meya kama binamu yake kuhusu masaibu ya umma pengine huenda akamsikiliza. (alama 4)

(b) **Tamathali za lugha**.

(i) Msemo – msikate tamaa.

(ii) Tashihisi – mlango huenda ukasalimu amri. (alama 4)

(c) **Kwa nini wanaorejelewa wanakaribia kukata tamaa.**
- Mishahara duni
- Kulipwa mshahara nusu na hata mshahara kukosekana hata baada ya miezi mitatu.
- Kukosekana kwa dawa hospitalini.
- Madiwani kuongezewa mishahara huku wao wakipuuzwa.
- Madiwani kutolipa kodi.
- Ufisadi – unyakuzi wa ardhi ya umma, kuuza fimbo ya meya.
- Kukosekana kwa ajira kwa vijana wanaofuzu.
- Hali duni ya usafi wa mazingira.
- Vifo vya wagonjwa hospitalini.

- Njaa – watu kukosa lishe kiasi cha watoto kulishwa kiporo.
- Kukoseakana kwa vifaa vya kufanyia kazi. (hoja zozote 8x1 = alama 8)

(d) **Sifa za Siki**.

- Mshauri mwema
- Mzalendo
- Anawajibika
- Ni mtetezi wa haki
- Mwenye kujali maslahi ya wengine. (alama 4)

Tanbihi: Lazima mtahiniwa atoe maelezo ya kudhibitisho sifa hizo.

3. **MEYA**

- Meya kulinganisha ufanisi wa Cheneo na wa miji midogo na dhaifu, badala ya kuendelea kupiga hatua mbele wanapiga hatua kinyumenyume.
- Meya kujifanya hajui watu wanateseka. Amefumba macho kwa matatizo yao kama mshahara duni n.k.
- Meya kukataa kuonana na kuwasikiza viongozi wa wafanyakazi, hata anapokutana nao anapuuza mapendekezo yao.
- Kuna baadhi ya watu wanaomuunga Meya mkono, hataki kujua juu ya wengi. Wachache wanatosha.
- Nyimbo za kizalendo kabla na baada ya vipindi muhimu, miaka hamsini baada ya uhuru.
- Mipango ya miaka kumi inapuuzwa. Meya anasema kuwa wana mipango ya miaka kumi ni upuzi.
- Afya bora nay a bure ilihaidiwa wananchi; wanalazimika kulipa.
- Wananchi hawakushikirishwa katika maamuzi. Wengine kama Siki kutimuliwa nyumbani mwa meya, wanapojaribu kumwelezea malalamishi ya Raia.
- Mikutano kufanywa kwa nadra, kama tunavyoelezwa na Diwani 1. Hufanywa hasa wakati kuna jambo kama mgomo kutokea.
- Ahadi za uongo – shehena ya dawa kuwa bahari kuu.
- Uchafu kuenea kila mahali na uvundo kukoleza hata ndani mwa nyumba.
- Kujiongezea mishahara kama overtime, marupurupu.

- Kula viapo vya kuficha siri za wizi ama wa fimbo ya meya.
- Meya kutojua kuwa hakuna maji safi. Anapoelezwa kuwa maji yanayotumika katika hoteli za mjini yanayosombwa kwa punda kutoka mtoni anastaajabu. (zozote kumi) (10 x 2)

4.
- Amani na Imani wanakutana safarini na wanaamua kuandamana hata kama mbeleni hawakujuana.
- Madhubuti ambaye ni wa tabaka la juu anatangamana na Amani na hata kuhamia kibandani mwa Amani ili waendeleze juhudi za ukombozi.
- Amani na madhubuti wanahimiza usawa na kutekeleza suala hili kwa kugawia maskini ardhi.
- Amani na Imani wanabadilika mtazamo wa watu kwa walemavu.
- Amani na Imani wanachangia kutekelezwa kwa haki na Yusufu Hamadi anatolewa lawamani.
- Amani anajua umuhimu wa msamaha na maridhiano. Anahimiza Ocar Kambona asilipize kisasi kwa Mtemi Nasaba Bora.
- Madhubuti anapendekeza jamii inayodumisha maadili. Anakataa kazi aliyotafutiwa na babake kwa njia ya ufisadi.
- Imani anapinga taasubi ya kiume anapomwambia Amani asiwaweke pembeni wanawake katika kitabu anachoandika.
- Wanafunzi wa chuo kikuu wanapambana na wizi wa kitaaluma kwa kumwaibisha majisifu na kumfanya abadilike.
- Amani na Imani wanapania jamii mpya inayolinda haki za watoto kwa kumlea mtoto Uhuru japo si mtoto wao.
- Amani na Imani wanapuuza miiko isiyofaa kwa kuyanywa maji ya mto kiberenge. (10x2 )

5. **RIWAYA – KIDAGAA KIMEMWOZEA**

(a) – Haya ni maelezo ya mwandishi akimrejelea mwalimu Majisifu. Hapa ni katika ukumbi wa chuo kikuu cha Mkokotoni ambapo mwalimu Majisifu aliposhindwa kuwasilisha mhadhara na kujichanganya umati ulipo fumukana baadhi yao walimjongelea mwalimu Majisifu ili angalau waweze kumsalimia mkononi au kupiga picha naye. (alama 4)

(b) Kinaya – mwalimu Majisifu si mwandishi bora hata alishindwa kujieleza. (alama 2)

(c)
- Ni kinaya kuwa zahanati ya Nasaba Bora inajulikana kama mahali ambapo watu wanakwenda kujifia.

- Ni kinaya kuwa dini zote zinahubiri amani, udugu na rehema lakini maovu mengi hutendwa katika jina la Mungu.

- Fao alijihusisha kimapenzi na mwanafunzi wake.

- Wasimamizi wa timu ya Songoa F.C. walimpuuza Chwechwe makweche baada ya kuvunjika fupaja.

- Maneno ya Balozi kuwa kuondoka kwa mzungu kulileta heri.

- Nasaba Bora kusema watu wengi watahudhuria mazishi yake.

- Uso wa Imani kuonyesha tabasamu siku zote.

- Nyumbani kwao Imani kunaitwa Baraka.

- Nasaba Bora kuwafuta kazi wafanyikazi walionadhifisha mazingira yake. (zozote 7x2)

6. (a) **<u>Majibu ya Damu Nyeusi – Ken Walibora</u>**

- Haya ni maelezo ya mwandishi kumhusu Fikirini.

- Anaeleza jinsi mwanamume huyu alivoykuwa anatembea katika kijia akielekea katika chuo kikuu kule nchini marekani.

- Hii ni baada ya kuachwa na basi la abiria lililokuwa linaendeshwa na dereva mzungu.
- Alimwacha Fikirini katika kituo rasmi cha basi maksudi.

- Hii ni kutokana na ubaguzi wa rangi uliokuwa huko kwa sababu Fikirini alikuwa mweusi (damu nyeusi bila shida.

- Baadaye Fikirini aliweza kuibiwa vitu na Fiona (mwanamke muamerika mweusi) baada ya kumdanganya Fikirini kuwa angempeleka chuoni. (alama 4x1 = 4)

(b) Anayerejelea hapa ni Fikirini na alikuwa anaenda chuo kikuu alikosomea. Alikuwa ni mwanafunzi wa somo la kiingereza katika chuo kikuu. (alama 1x2 = 2)

(c)

- Alikuwa mlevi. Akiwa Afrika mashariki. Alitembea sehemu mbalimbali katika nchi ya Kenya, Tanzania na Uganda akitafuta pombe a aina mbali mbali.

- Mvumilivu – alivumilia kuulizwa maswali ya ajabu na wahadhiri na wanafunzi amani waliokuwa wazungu.

- Alikubali mambo haraka – Fiona alipomwambia kuwa angempeleka chuoni kwa gari lake alikubali akamfuata haraka na kuingia ndani ya nyumba bila kuomba asubiri nje.

- Ni mtamaduni – Alipenda vyakula vya kiafrika sana kuliko vya marekani.

- Mwenye bidii – alipoachwa na gari la abiria anaamua kutembea kwa miguu akielekea chuoni badala ya kurudi chumbani pia kusoma hadi kwenda kutafuta elimu ya juu Amerika.

- Alikuwa na upweke – alipomwona Mwafrika mweusi kama yeye nchini Amerika alitamani awe rafikiye.

(alama 6)

(d) **<u>Umuhimu wa Fikirini</u>**

- Ametumiwa na mwandishi kuonyesha jinsi wafrika wanavyodhulumiwa na wazungu. Fikirini alibaguliwa chuoni, barabarani na mkahawani.

- Anatumiwa na mwandhishi kuonyesha umuhimu wa kutia bidii katika masomo na kufikia viwango vya juu.

- Ni kielezo cha watu wavumilivu katika jammi. Akiwa Amerika alivumilia dhuluma za aina mbalimbali alizotendewa na jamii ya Amerika.

- Ni kiwakilishi cha watu walio na mapenzi kwa nchi zao anapenda nchi za Afrika mashariki sana. Hii ni ishara ya uzalendo kamili.

- Anatumiwa kama kielelezo cha watu wanaopenda utamaduni wao, vileo chakula n.k.

(zozote 5x1 = 5)

(e) **<u>Mbinu za lugha</u>**.

(i) Tanakali za sauti Ananyapianyapia nyapu nyapu na kupepesuka pepesu.

(ii) Tashbihi Mf. Ananyapia nyapu nyapu na kupepesuka kama mlevi chakari.

(iii) Taswira Mwandishi anatupatia picha ya jinsi Fikirini alivyokuwa akitembea kama mlevi juu ya barafu.

(iv) Tanakali ya sauti Mlevi chakari. (zozote 3x1 = 3)

7. **<u>Mzizi na Matawi – Ali Abdula Ali</u>**

(a)

- Bi.Mkubwa (mama mtu)
- Ni mdanganyifu / mwongo.

Anadanganya Sudi kuwa baba yake alikuwa amefariki kabla ya kuzaliwa kwake.

- Ni mkarimu. Alimlea sudi akamwelimisha hadi ng'ambo kisha akampa nyumba yake airithi.

- Ni mwenya kuomba msamaha. Alimwomba msamaha Sudi kwa kumdanganya siku nyingi kuhusu asili na fasili yake.

- Ni mwenye huruma / utu: utu unamfanya kumchukua Sudi katika pipa la taka na kumlea kama mtoto wake.

- Msiri: Hakumfichulia Sudi kuhusu usawa wake. Alimdanganya umuhimu.

- Kielezo cha watu wenye ukarimu: anamlea Sudi kama mwanawe na kumrithisha.
- Kielelezo cha watu ambao husema ukweli baadaye bila kujali athari yake. Kumjua Sudi kuhusu usawa wake. (sifa alama 2 umuhimu alama 1 = 3)

(ii) **Bi Kidura**.

- Ni katili – ukatili wake unadhihirika anapowatupa Sudi katika pipa la takataka baada ya kumzaa aendelee na ana za ujana.

- Ni mcha Mungu – alimwomba Mungu msamaha kwa sababu ya dhambi ya kutupa mtoto wake baada ya kumzaa.

- Ni mwenye bidii. Alifanya kazi ya nyumbani kwa Bi. Mkubwa. Alimpikia, akafagia, akamfulia, akapiga deki n.k.

- Mpenda anasa – alimtupa mtoto wake mchanga kwenye pipa la takataka aendelee na anasa za ujana.

- Mwenye shukrani – aliwashukuru Sudi na Bi. Mkubwa kwa kumruhusu aishi nao. (alama 2)

**Umuhimu**

- Anaendeleza maudhui ya majuto. Anajuta baadaye kwa kumtupa mwanawe.

- Mwandishi anamtumia kuwaonya watu dhidi ya maamuzi mengine maishani: kumtupa mtoto.

- Kielelezo cha majuto kwambo mambo tufanyayo huweza kuleta majuto baadaye.

- Kielelezo cha utamaduni uliopitwe na wakati wa kutotaka kujulikana alikuwa na mtoto. (alama 1)

**SUDI ABDALA**

(i) Mwerevu – alisoma kwa bidii na kupata shahada ya udaktari wa wanasheria ulaya.

(ii) Mkarimu – ukarimu wake ulimfanya ampatie Bi. Kidura kazi na akaagiza apewe chakula, malazi na nguo.

(iii) Mpenda anasa – anaenda katika karamu ya sikukuu ya pasaka na kucheza densi na waridi. Pa alienda Tea Breeze akiwa na Radhia kustarehe huko.

(iv) Hakati tamaa. Hakukata tamaa ya kumuuliza Bi. Mkubwa kuhusu aliko baba yake.

(v) Jasiri. Anarudi nyumbani peke yake usiku bila uoga wowote.

(vi) Ni msamehevu. Anamsamehe Bi. Mkubwa kwa kumdanganya kuhusu baba yake. Alikuwa anamdanganya kuwa baba yake alikuwa ameaga dunia. Alimsamehe Bi. Kudura kwa kumzaa na kumtupa katika tupa.

(vii) Mwenye bidii – Alitia bidii akasoma hadi chuo kikuu udaktari katika wanasheria.

(viii) Mwenye kutafuta ukweli – mara kwa mara alikuwa anamuuliza Bi. Mkubwa kuhusu fasili na asili yake. Alikuwa anamuuliza mara kwa mara kwa sababu hakuridhishwa na jibu alilokuwa akipewa na mama huyu. (alama 2x1)

**Umuhimu**

i. Kielelezo cha vijana wenye heshima na bidii inayowainua maishani.

ii. Anatumiwa na mwandishi kuonyesha umuhimu wa kuwa na mtoto. (alama 2)

(b) **Maudhui ya mapenzi**.

- Bi. Mkubwa (Mama Mtu) na Bw. Abdalla walikuwa na mapenzi ya dhati. Bi. Mkubwa anamweleza Sudi kuwa walioana na Abdalla aliyekuwa mwarabu wa kutoka Mauye na kuishi kwa mapenzi kama mke na mume. Lakini mapenzi yao hayakudumu kwani Abdalla aliweza kufariki na kumwachia mkewe na mimba ya Sudi.

- Sudi alionyesha mapenzi kwa wasichana. Alipendwa sana na wasichana/ alipendwa sana na wasichana kwa urembo wake na utanashati.

- Sudi alipendwa na wanawake alipokuwa katika sherehe za karamu ya Pasaka Easter get together.

Walitaka kucheza densi naye. Hangeweza kucheza na wote.

- Bi. Mkubwa anamwonyesha Sudi mapenzi ya kiwango cha juu. Aliutunza na kumlea Sudi vizuri na kumsomesha hadi akapata shahad a ya udaktari wa sheri.

- Bi Kidura alionyesha mapenzi kwa Sudi alipoajiriwa kwa Bi. Mkubwa hadi akashika uhusiano wake na Sudi. (5x2 = alama 10)

8. **FASIHI SIMULIZI**.

(a) Maana ya maghani

- Mashairi ya kukaririwa tu hayaimbwi.

- Hutolewa kwa kalima badala ya kuimbwa. (alama 2)

(b) **Sifa za maghani**.

- Ni tungo la kishairi. Yaani yana muundo wa ushairi.

- Husimulia matukio kwa kirefu hasa yanayotambwa.

- Hutungwa papo hapo na kusemwa mbele ya hadhira.

- Hutungwa kwa ufundi ukubwa.

- Huweza kutolewa na mtu mmoja au kundi ki watu.

- Anayeghani hujisifu / kusifu kitu / jambo fulani.

- Huwa na majigambo mengi.

- Huambatana na ala mbalimbali za muziki. (alama zozote 6x1 = 6)

(c) **Aina tatu za maghani**.

- Tondozi – Tungo zinazoghanwa na huwasifu watu, wanyama na vitu.

- Tendi - Huitwa pia ushairi wa ushujaa. Hujumuisha sifa zinazoonyehsa mafanikio ya mashujaa na mbolezi zinazoonyesha anguko la shujaa / mtawala.

- Rara – hadithi fupi na nyepesi za kishairi zinazopitishwa kwa mdomo.
- Huzungumzia tajriba ya maisha.

- Pembezi – Ni aina ya tondozi inayotolewa kusifu watu fulani pekee mf. viongozi, waganga mashuhuri, waelezi wazuri, wapenzi waliopigania pendo lao n.k.

- Sifo – Ni mashairi ya sifa ambayo hughanwa kumsifu mtu fulani kutokana na matendo yake ya kishujaa (zozote 3x2 = 6)

(d) **Umuhimu wa maghani**.

- Kuburudisha: husisimua hadhira.

- Kuelimisha: huwaelimisha wanajamii kuhusu utamaduni wao.

- Husifu tabia hasa ya watu wenye tabia za kishujaa.

- Hukashifu tabia potovu ili kuwakosoa wanaohusika.

- Huhifadhi historia ya jamii – ili watu kuonea fahari jadi yao.

- Huendeleza lugha: Huimarisha stadi ya kuongea na kukuza ujasiri wa kuongea hadharani.

- Hueneza umoja / ushirikiano katika jamii watu hujumuika pamoja kusikiliza maghani na hii huleta utangamano. (zozote 6x1 = alama 6) Tanbihi: Mtahiniwa asipoelezea umuhimu hadhibiwe.